**JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

**Kumb Na. DCC/AE.16/2** **10/11/2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam anawatangazia Watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Jiji hili, kuomba nafasi za kazi kumi (10) baada ya kupokea kibali kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao: -

### 1. DEREVA DARAJA LA II - NAFASI 10

### 1.1. MAJUKUMU YA KAZI YA DEREVA II

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
iv. Kutunza na kuandika daftari la safari “log book” kwa safari zote
v. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
vi. Kufanya usafi wa Gari
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

### 1.1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya Daraja la C au E ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka

mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au NIT au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.3 NGAZI YA MSHAHARA

**TGS B**

### MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45;
ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya ulemavu walionao.
iii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili;
iv. Waombaji ambao tayari ni Waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. **CCA. 45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010**.
v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
vi. Waombaji wa kazi ya Dereva Daraja II wenye leseni Daraja E au C wanapaswa **KUAMBATISHA** vyeti vya udereva vilivyo wapatia sifa ya kupata madaraja husika.
vii. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho cha elimu pamoja na cheti cha mafunzo ya Udereva na Ujuzi, Testmonials Provisional Results Statement of Rusults hati matokeo za kidato cha nne na sita (**FORM IV FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
viii. Waombaji walisoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**)

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

x. Waombaji wenye majina tofauti katika vyeti vya Taaluma, Kuzaliwa na NIDA waambatishe **DEED POLL**

xi. Waombaji wenye tofauti za herufi katika vyeti vya Taaluma, Kuzaliwa na NIDA waambatishe **Hati ya kiapo cha majina (Affidavit)**

xii. Waombaji watakao wasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.

xiii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **24/11/2025.**

xiv. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**

**MUHIMU**: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu kwenda kwa;

**MKURUGENZI WA JIJI,**
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM,**
**S. L. P 20950,**
**DAR ES SALAM.**

*Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal kupitia anuani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa ‘“Recruitment Portal’*

**Limetolewa Na: -**

*Elihuruma S. Mabelya*
**MKURUGENZI WA JIJI**